


**HABARI KITAIFA**

# WHI yatakiwa kubuni nyumba za watumishi wa umma

## Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameitaka Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI) kuja na ubunifu wa kujenga makazi bora ya watumishi wa umma katika maeneo ya mijini jirani na maeneo ya shule na hospitali ili kuwaondolea changamoto ya makazi manesi na walimu na kuboresha utendaji kazi wao.

Amesema maeneo ya mijini, shule pamoja na hospitali zinamiliki maeneo makubwa ambayo Taasisi ya WHI inaweza kuyatumia kujenga majengo marefu kwenda juu ili kuwafanya walimu na manesi wafurahie kutoa huduma kwa wananchi kwa kuishi kwenye makazi bora jirani na maeneo

ya kazi.

Simbachawene alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na timu ya menejimenti ya WHI ikiwa ni mwendelezo wa kusikiliza changamoto zinazoikabili taasisi anazozisimamia pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo aliyyoatoa wakati wa ziara aliyoifanya mwezi Agosti, mwaka jana. Alisema katika maeneo ya mijini watumishi wakiwamo walimu na manesi wanalazimika kutafuta makazi mbali na maeneo wanakofanya kazi kwa vile ni vigumu kupata nyumba na hata zikipatikana gharama zake ni kubwa kulingana na kipato chao.

"Hakuna asiyejua umuhimu wa walimu na manesi katika nchi hii, lakini wengi wamekuwa wakiishi maeneo ya mbali na wanakofanya kazi na kuzimika kulipa nauli kubwa kwa

vile hawawezi kumudu kulipa kodi ya makazi yaliyo jirani na maeneo yao ya kazi, waguseni hawa kwa kuwajengea makazi bora," alisema.

Alisisitiza kuwa nyumba zikiwa jirani na eneo la kazi inasaidia kupunguza gharama za maisha na kuongeza ufanisi kazini na hilo ndio lengo la serikali kuhakikisha watumishi wanafurahia mazingira ya kazi kwa gharama rafiki.

Alisema watumishi wa umma wakiwamo walimu na manesi wanaofanya kazi katika maeneo ya mijini wanalazimika kusafiri umbali mrefu kutoekana na changamoto ya makazi na kusababisha kutoa huduma zisizoridhisha kwa wateja wao.

Kadhalika, kitendo cha watumishi wa umma kutoekwa na makazi bora na kuwa mbali na maeneo yao ya kazi

ni changamoto kubwa inay-oathiri utendaji kazi na kuitaka taasisi hiyo kuona umuhimu wa kufanya hivyo kwa kuwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025.

Alisema ujenzi wa makazi bora karibu na maeneo ya kazi, utawasaidia watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kutohangainka.

"Mkijenga nyumba maeneo ya jirani na vituo vya kazi, kutawasaidia sana watumishi kutoichukia kazi kwa kuwa watapata sehemu nzuri ya kuisi," alisitisiza.

Mkurugezi wa Taasisi ya Watumishi Housing, Dk. Fred Msemwa, alisema kwa mwaka 2023/24 imeendelea na ujenzi wa nyumba Njedengwa, Magomeni na Gezaulole ili kupunguza adha wanazopitaa watumishi wa umma wakiwamo walimu na manesi.